# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA TANO

**03 FEBRUARI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA TANO – TAREHE 03 FEBRUARI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

### 70. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Mikoa mingapi ina Vituo vya kuwezesha Wananchi kiuchumi, huduma zipi zinatolewa na Wananchi wangapi wananufaika.

### 71. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutengeneza uendelevu kwa Vijana wanaonufaika na programu mbalimbali za kukuza ujuzi na stadi za kazi.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 72. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kufanya ukarabati wa Barabara za Mitaa ili kuondoa usumbufu unaojitokeza wakati wa mvua.

**73. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itarejesha mawasiliano ya Barabara kati ya Mkangala – Kawawa – Namahyakata katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

**74. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule ya Sekondari ya Wasichana katika Jimbo la Mwibara.

**75. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Ofisi ya Ardhi Wilaya ya Nyasa itapatiwa gari ili kudhibiti uendelezaji holela hasa katika Mji wa Mbamba Bay.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**76. MHESHIMIWA MUHARAMI SHAABAN MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itajenga Kingo za Mto Mpiji zilizopanuka kutokana na mvua kubwa na kuhatarisha nyumba za wananchi wa maeneo hayo.

**WIZARA YA NISHATI:**

**77. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji vya Msamba - Masokolo, Izinga, Lyele na Vitongoji vya Kisenga na Lupata vilivyopo Kijiji cha Lyapinda.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**78. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha ongezeko la Vyombo vya Habari Mtandao haliathiri maadili na utamaduni wa Taifa letu.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**79. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali italeta mabadiliko ya Sheria ya Kuasili Watoto kwani iliyopo imepitwa na wakati.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**80. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatenga eneo la sehemu ya Hifadhi ya Mto Ugala ili Wananchi waweke Mizinga ya Asali.

## WIZARA YA UJENZI:

**81. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga upya Barabara ya Masasi – Mingoyo hadi Mtwara.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**82. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itanunua gari la Zimamoto Wilaya ya Ngorongoro.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**83. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini TMA itafanya kazi na Idara ya Mazingira ili kusaidia Sekta nyingine kupambana na athari za mabadiliko ya Tabianchi.

## WIZARA YA AFYA:

**84. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itaongeza kasi ya upatikanaji wa huduma kwa Watu wenye Magonjwa ya Damu kama Hemophilia na Seli Mundu.

**85. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Wataalam wa Afya ya Akili nchini.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**86. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya katika Mji wa Ilongero - Singida.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

### 87. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga Soko la Kisasa la Samaki katika Mji Mdogo wa Somanga - Kilwa.

## WIZARA YA KILIMO:

### 88. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka ukomo wa bei za Mbegu za Mahindi ili kuondoa upandishaji holela wa bei.

### 89. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukwamua mdororo wa bei ya Zao la Muhogo - Muhambwe.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**DODOMA**
**03 FEBRUARI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**